

LISTEN TO "MITIKI YETU" ON RADIO PAMBAZUKO 89.5 FM EVERY FRIDAY 19:30-20:00 & SATURDAY 07:30-08:00

KVTC SINCE 1992

Kutoka kwa Dawati la Irvine:

Kipindi cha Mwaka 2022-2023 kimekuwa chenye shughuli nyingi za mafanikio kwa KVTC. Tumeanza vizuri, tunatumaini tutaendeleza mafanikio hayo. Makala hii inaelezea miradi mbali mbali ambayo tumetekeleza. Tafadhali furahia makala hii na tunaomba maoni yako.

## Utafiti Wa Hadhi Ya Juu Ya Uhifadhi Katika Eneo La KVTC.

**Na Joseph John**


KVTC inasimamia ardhi yenye ukubwa wa hekta 28,132. Takribani 30% ya ardhi imepandwa miti ya Mitiki na 70% takribani hekta 20,000 ni uoto wa asili na unahifadhiwa.

Hifadhi ya KVTC ina mchango mkubwa katika eneo hili na inatumika kama ushoroba wa wanyamapori kati ya milima ya Udzungwa na hifadhi ya taifa ya Nyerere. Imekuwa pia makimbilio ya wanyama pori na pia ina thamani ya juu ya bioanuwai.

Mnamo Mwezi Septemba 2022 KVTC ilitangaza tenda ya uwasilishaji mapendekezo ya kufanya tathimini ya Misitu yenye thamani ya juu kiuhifadhi ndani ya eneo lake. Utafiti huu unatimiza mahitaji ya kukidhi viwango vya kimataifa vya misitu duniani (FSC).

Lengo la utafiti huu ilikuwa ni (i)Kutambua maeneo yenye thamani ya juu ya kiuhifadhi kulingana na zana za HCVRN. (ii) Kutoa mwongozo wa namna ya kusimamia maeneo ili kudumisha au kuboresha hadhi ya uhifadhi. (iii) Kutoa mwongozo wa mbinu na vipindi vya ufuatiliaji wa hali ya maeneo yenye hadhi ya juu ya uhifadhi yaliyotambuliwa.

Mnamo mwezi Januari 2023, utambuzi wa maeneo yenye hadhi ya juu ya uhifadhi (HCVA) ulifanywa na timu ya wataalamu kutoka kampuni ya Environmental Forest Certification Limited (EFC). Utafiti huu ulihusisha uchoraji shirikishi wa ramani na kutathimini maeneo yenye hadhi ya juu ya uhifadhi na kuyarejelea kijiografia kupitia mfumo wa GIS. Utambuzi huo uliwashirikisha wadau mbalimbali kutoka jamii za wenyeji hadi wataalam wa ngazi ya juu na uhakiki wa kina wa taarifa bora zilizopatikana.
Utafiti huo ulithibitisha kuwa, ardhi ya KVTC ina hadhi zote za juu za uhifadhi (HCVs) kulingana na mfumo wa uainishaji ulioandaliwa na Mtandao wa rasilimali za hadhi ya juu ya kiuhifadhi (HCVRN).
Makundi sita tofauti yanawakilisha viwango vya juu vya thamani ya uhifadhi vinavyopaswa kuhifadhiwa, ikiwa ni pamoja na mchango wa usimamizi wa KVTC na wadau husika ili kuokoa kiasi cha mwisho cha hadhi ya juu cha uhifadhi kilichobaki ndani ya ardhi ya KVTC.




Utafiti ulishauri kuwepo kwa mbinu mbalimbali na programu za ufuatiliaji ili kulinda makundi sita ya hadhi ya juu ya uhifadhi (HCVs) ambapo itaimarisha kuwepo kwa aina adimu ya viumbe hai vinavyotishiwa na viko hatarini kutoweka ambavyo ni mimea na Wanyama; pamoja na kutoa hifadhi kwenye maeneo ya ardhi isiyolindwa.
Ripoti kamili ya utafiti wa hadhi ya juu ya kiuhifadhi (HCV) inaweza kupatikana kwenye tovuti ya KVTC. https://www.kvtc.co.tz.

## KVTC Ni Chaguo La Waajiriwa Zawadi ya mfanyakazi Bora


**Na James Njaala**

KVTC inatambua utendakazi wa wafanyikazi wake na juhudi wanazoweka ili kufikia malengo ya kimkakati ya kila mwaka ya kampuni. Utambuzi huo unaenda mbali zaidi ya desturi ya kawaida ambapo KVTC hufanya zoezi la kuthamini utendaji kutoka kwa kila sehemu ya shughuli zake kuu. Kila mwaka tuna wafanyakazi 8 bora zaidi, na kila mfanyakazi bora hupewa tuzo nzuri sana.

Wafanyakazi bora kwa mwaka 2022 ni **Shafii Tundua** - Opereta, **Sadick Lidwaku** - Karani wa Hesabu za magogo, **Msigwa R. Msigwa** - Kiongozi wa Kitalu cha Uzalishaji miti, **Frank Mhomanga** - Mhudumu wa Drymill, **Stella William Kweka** – Mhasibu Msaidizi; **Sudi Mpandule** – Fundi matengenezo, **Japhet Nyamaru** – Opereta wa logger na **Mwajuma Kaswaga** – Mhudumu wa kuchambua Mbao

***Mfanyakazi Bora Zaidi kwa mwaka 2022:***
Miongoni mwa wale wafanyakazi 8 hapo juu, uongozi wa KVTC kupitia kamati ya wakuu wa Idara huchagua mfanyakazi bora zaidi wa

jumla wa mwaka husika. Mwaka wa 2022 mfanyakazi bora zaidi alikuwa **Stella William Kweka** – Mhasibu Msaidizi kutoka idara ya Fedha. Stella ni mfanyakazi wa KVTC kwa zaidi ya miaka 6 sasa. Maadili ya kazi yake hayana shaka. Ana huduma bora kwa wateja kuliko kila mtu. Yeye ni wa kipekee na anastahili pongezi kutoka kwa kila mmoja hapa KVTC.



*Stella Kweka*

## Mradi Wa Maboresho Ya Bustani Ya KVTC

**Na Jeremiah M. Gumadi**

Ni miaka 10 sasa tangu KVTC ilipodhamiria kuanza mchakato wa kuongeza faida ya mauzo ya mitiki (misaji) pasipo kuongeza eneo la upandaji. Ushahidi wa kisayansi unadhihirisha ongezeko la faida lenye mashiko linaweza patikana pale tu mbegu bora itatumiwa sambamba na matunzo sahihi ya miti.

KVTC inaendesha wa utafiti wa mbegu bora za mitiki tangu 2013/14. Huu ni mradi mkubwa wa aina yake kati ya miradi mikubwa barani Afrika. Uwekezaji huu mkubwa ulifuatia baada ya jaribio la awali la 2003/04 ambalo lilihusisha miche-vikonyo bora vya mitiki kutoka Malaysia na mbegu za kawaida ambazo zimekuwepo nchini kwa vizazi. Mradi huu unaitwa **MRADI WA ONGEZA 20** wenye lengo la kuongeza faida ya KVTC kwa asilimia 20



*Miche Mama*

**MRADI WA ONGEZA 20** unahusisha majaribio ya vikonyo na mbegu katika vitalu 7. Vyanzo mbali mbali vya mbegu za kawaida kutoka mashamba ya KVTC ambazo zimekuwepo nchini kwa vizazi, Malaysia, Australia, Thailand, Brazil, Costa Rica and India vinajaribiwa. Vitalu majaribio hivi hutunzwa vizuri na vipimo vya mwenendo wa ukuaji wa miti hufanyika kila mwaka. Aidha, vipimo vingine vya sifa muhimu za uzalishaji mbegu bora kama utoaji wa maua, unyoofu wa mti, unene wa matawi na mapango kwenye shina la mti hufanyika. Pia vipimo vya sifa muhimu za uzalishaji mbegu bora kwa ajili ya masoko kama tabia anuai za mbao, rangi ya kiini cha mbao na kimo cha mti kinachofaa kukata magogo hufanyika.

Ili kutimiza ndoto ya **MRADI WA ONGEZA 20** mambo mawili muhimu hayana budi kufanyika:

i. Uchakataji makini wa kisayansi wa takwimu zinazokusanywa kutoka katika vitalu majaribio ukifuatiwa na upangaji wa miti katika madaraja kwa kuzingatia vigezo maalum vya mbegu bora na kuhitimishwa kwa kuchagua miti bora zaidi
ii. Kurudufu/nakili kwa wingi kwa njia ya vikonyo miti bora iliyochaguliwa kwa ajili ya majaribio zaidi sambamba na kupanda mashambani kwa uzalishaji wa mitiki wenye tija zaidi

Kwa kushirikiana na mtaalam wa kuzalisha mbegu bora za miti Dr. Andrew Callister kutoka Marekani, KVTC imefanikiwa kukamilisha kipengele cha kwanza. Hivi karibuni mtaalam mwingine wa kuzalisha mbegu bora Prof. Olman Murillo kutoka Costa Rica anashirikiana na KVTC kukamilisha kipengele cha pili.

Mafanikio ya kipengele cha pili yana uhusiano wa asilimia 100 na bustani ya miti. Kunahusisha hali ya mpito kutoka uzalishaji uliopo sasa wa miche bora ya kawaida ya vijiti takribani **600,000** kuelekea uzalishaji wa kimataifa wa miche-vikonyo bora vilivyopatikana kwa uchaguzi umakini. Hali hii ya mpito inalazimu maboresho makubwa ya miundombinu kwenye bustani iliyopo.

Maboresho muhimu ya miundombinu yatakayofanyika kwa awamu ndani ya miaka miwili ijayo ni:

i. Mabanda vitalu manne na vifaa vyake vyote muhimu kwa ajili ya kutunzia nakala za miti ya mbegu bora na kwa kuzalishia miche-vikonyo
ii. Mabanda maalum na vifaa vyake vyote muhimu kwa ajili ya kukomazia na kuhifadhia miche-vikonyo kabla ya msimu wa upandaji mashambani kuwadia
iii. Miundombinu ya kuvunia na kuhifadhia maji ya kutosha
iv. Maboresho mengineyo muhimu ya miundombinu kwa ajili ya mazingira bora zaidi ya kufanyia kazi

Maboresho yameshaanza na yanaendelea kwa kadri ya mpango mkakati. KVTC inatarajia kuondokana na uzalishaji uliopo sasa wa miche bora ya kawaida ya vijiti kwa awamu ndani ya miaka mitatu. Itajikita na uzalishaji wa kimataifa wa miche-vikonyo bora takribani **600,000** kwa mwaka.



*Banda Kitalu*

Hata hivyo, maboresho ya miundombinu yalitanguliwa na kujenga uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi. Mwaka jana Mkuu wa Idara ya Misitu na Meneja Utafiti walipata wasaa wa kusafiri nchini Costa Rica kujionea aina mbalimbali za uanzishaji na uendeshaji wa bustani za kisasa za miche-vikonyo bora. Pia wataalam wa kimataifa wa kuzalisha mbegu bora za miti walitembelea KVTC kwa mashauriano zaidi. Mapema mwaka huu pia Meneja Msaidizi wa Bustani alipata wasaa wa kwenda nchini Cost Rica kwa majuma mawili kuona na kujifunza kwa vitendo mbinu za uendeshaji wa bustani na uzalishaji wa miche-vikonyo bora kisasa.

Tafiti za mbegu bora ni jambo nyeti na endelevu kwa kampuni yoyote inayojiendesha kibiashara kwenye tasnia ya misitu na iliyojidhatiti katika kuzalisha mitiki yenye thamani kubwa na kwa tija kubwa kama KVTC

***Magogo Ya KVTC: Kuanzia Uvunaji Mpaka Uzwaji***

Na Geofrey Isaac Kessy

***MAGOGO YA KVTC: KUANZIA UVUNAJI MPAKA UUZWAJI***

***Uvunaji:***

*KVTC inavuna misitu yake kwa njia endelevu na kwa sababu hiyo nyayo zake za kibayolojia ziendelee kuwepo milele, kiasi cha uvunaji huu endelevu ni karibu mita za ujazo 35,000 hadi 40,000 kwa mwaka na inaonyeshwa kuongezeka hadi Zaidi ya 50,000 katika miaka ijayo, ikiwa ni jumla ya upunguzaji au mavuno ya mwisho kwa pamoja. Kiasi hiki huvunwa kutoka katika mojawapo ya vitalu vinne vilivyopo katika wilaya za Malinyi, Ulanga au Mlimba, Mkoa wa Morogoro.*

*KVTC hutumia wakandarasi kwa zaidi ya asilimia 70 kwa shughuli za uvunaji ambao hutumia mashine maalum za kukata na kukusomba magogo kwenda tayari kupelekwa kiwandani. Aidha baadhi ya kazi hufanywa na wafanyakazi kwa mikono. Miti huchakatwa kwa urefu tofauti wa magogo kutoka mita 2.5, 2.3 hadi kiwango cha chini cha mita 1.5.*

*Mkandarasi wa usafirishaji, Master one mwenye malori 8 ameajiriwa na KVTC kusafirisha magogo kutoka msituni hadi kiwandani. Kila lori lina uwezo wa mita za ujazo 13 za magogo. Malori hupakiwa kwa kutumia mashine ya Bell (mali ya KVTC.*



*Machine maalum ikipakia magogo kwenye lori kupeleka kiwandani*

*Shughuli zote za uvunaji usimamiwa na meneja wa uvunaji Amidu Yahaya ambaye nae anasimamiwa na Geofrey Kessy, Meneja Mkuu wa Misitu.*

***Upimaji na uuzwaji wa magogo:***

*Sehemu ya KVTC ya vipimo na mauzo ya magogo ina wapimaji 8 na waendeshaji 3 wa machine za logger ambao wanasimamiwa na Meneja Maria Mrema. Bell loggers hizo hutumika kwa ajili ya kupakua, kupanga, au kusogeza magogo kutoka eneo la kuhesabia mpaka maeneo ya wateja au kulisha kiwanda cha KVTC. Kila gogo hupimwa urefu na kipenyo kabla ya kupangwa katika madaraja tofauti*

*Kati ya jumla ya kiasi kinachovunwa, KVTC kwa sasa inauza karibu asilimia 60 ya mavuno hayo kwa viwanda vya nje na asilimia 40 inachakatwa na kiwanda chake. HIvi sasa kuna viwanda 6 vinavyonunua magogo kutoka KVTC. Mauzo ya magogo kwa viwanda vya nje hufanyika kwa njia ya mnada kila robo mwaka. Wazabunii wenye bei ya juu hupewa kipaumbele. Mchakato huu unasimamiwa na kamati iliyochaguliwa ambayo inajumuisha Mkurugenzi Mtendaji wa KVTC, Meneja Mkuu wa Misitu na Meneja wa fedha. Njia hii ya mauzo ya magogo imeonyesha matokeo mazuri mno mpaka sasa.*

## Mkusanyiko wa Picha



*Tony Finch na Geofrey Kessy wakiwa KVTC chini ya mti mrefu wa mtiki wenye umri wa miaka 18*




*Mashine ikinoa misumeno*



*Ujazaji wa vitalu vya miche*



*Mashine ya kuchakata mbao*



*Wafanyakazi bora wa mwaka 2022*



*Stoo ya bidhaa za mbao tayari kwa mauzo*



*Washiriki wa Mashindao ya uchoraji 2022 - Shule ya Sekondari ya Iragua*